

## **KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO YARIDHISHWA NA UTEKELEZAJI WA MRADI WA EASTRIP ATC**



Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, Tarehe 21/10/2023 ilitembelea Chuo cha Ufundi Arusha (ATC) kamapsi ya Kikuletwa na kukagua mradi wa kujenga ujuzi na ushirikiano Afrika Mashariki (EASTRIP) unaotekelezwa, pamoja na kupokea taarifa ya Maendeleo ya mradi.

Kamati hiyo ilipokelewa na Naibu Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia Mhe. Omar J. Kipanga na Mkuu wa Chuo cha Ufundi Arusha, Dkt. Musa N. Chacha, ambao kwa pamoja walitembelea mradi unaoendelea kutekelezwa ukiwemo mradi wa ujenzi wa majengo ya madarasa, karakana, mabeni Pamoja na ukumbi wa mihadhara inayofadhili na serikali kupitia Benki ya Dunia.

Akizungumza mara baada ya kukamilisha ziara ya kukagua miradi, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, Mhe. Husna Juma Sekiboko, amepongeza jitihada kubwa za uongozi wa Chuo katika utekelezaji wa Mradi na kuitaka Serikali kupitia Wizara ya Elimu, kuangalia namna bora ya kuongezea nguvu mradi huo ili kukamilika kwa wakati.

Kimsingi tumetembelea maeno mengi tumejionea wenywe kile ambacho mnatekeleza wenyewe kwenye Chuo hiki. Niwapongeze mradi unatekeleza Pamoja na changamoto nyingi ambazo tulielezwa kwenye kikao tukiwa Dodoma n ahata tulipofika hapa unachangamoto nyingi ambazo zimesababisha mradi kuchelewa lakini kifupi mnafanya vizuri, viwango ni vizuri, tunaridhika na utekelezaji wa mradi unakwenda vizuri alisisitiza

Naye Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Omar J. Kipanga, ameishukuru Kamati hiyo kwa kutembelea Chuo cha Ufundi Arusha, Kampasi ya Kikuletwa, na kuahidi Wizara itatekeleza maoni., ushauri, mapendekezo na maagizo yote ya kamati ili kufanyia kazi na kuboresha huduma zitakazo tolewa na chuo cha Ufundi Arusha.

Akiwasilisha taarifa ya Chuo kwa Kamati, Mkuu wa Chuo Dkt. Musa Chacha amesema, ujenzi wa Jengo la Huduma za mionzi katika Hopsitali ya Chuo umegharimu Tshs. Bilioni 3.4 na tayari umekamilika kwa asilimia 62.

#####

#